

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

**BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA YAIPATIA TANZANIA MKOPO NAFUU
WA SH.BILIONI 589.3 KUJENGA BARABARA KIGOMA**

Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zimesaini Mikataba miwili ya mkopo wenye masharti nafuu wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 256.2 utakaotolewa na Benki hiyo (takribani shilingi bilioni 589.3) kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu(KM 260) kwa Kiwango cha lami na Uboreshaji wa Miundombinu ya Huduma za Jamii.

Akizungumza baada ya kusaini mikataba hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Doto James ameishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania za uwekezaji katika miundombinu ya usafiri nchini.

"Benki hii imekuwa mshirika wa muda mrefu wa Serikali katika maendeleo ya miundombinu na uwekezaji wake umekuwa wenye ufanisi na matokeo ya kuridhisha" Alisema Bw. James.

Alisema kuwa utekelezaji wa mradi wa barabara wa Kabingo -Kasulu -Manyovu ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano, ambao unalenga kuimarisha miundombinu ya usafiri ili kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kupunguza umasikini na kuimarisha ushirikiano wa kikanda.

"Barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu ni kiunganishi muhimu katika maendeleo na uboreshaji wa biashara ndani na nje ya nchi. Mradi wa ujenzi wa barabara hii utakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya Rumonge - Gitaza (km-45) nchini Burundi ili kuboresha mtandao wa barabara za Afrika Mashariki" Alisisitiza Bw. James

Bw. Doto James, ambaye pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, alifafanua kuwa mradi wa ujenzi wa barabara hiyo utakapokamilika utaunganisha Bandari ya Dar es Salaam na mikoja ya magharibi mwa Tanzania na kufungua masoko ya kikanda nchini Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

"Aidha, mradi utachangia katika kupunguza gharama za uendeshaji magari, kuboresha usalama wa barabara, kupunguza gharama zingine za usafirishaji na uboreshaji wa upatikanaji wa miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi kwenye maeneo ya mradi mkoani Kigoma" alibainisha Doto James.

Bw. James alisema kuwa, mbali na ujenzi wa mradi wa barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu, mkopo huo pia utahusisha uboreshaji wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ili kifikie hadhi ya kituo cha umahili wa usalama barabarani katika Kanda ya Afrika Mashariki ;Ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha katika Mpaka wa Manyovu (Tanzania) / Mugina (Burundi), na uboreshaji wa miundombinu ya huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na ukarabati wa masoko ; Usambazaji wa maji na usafi wa mazingira.

Kwa upande wake, Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Dkt. Alex Mubiru aliishukuru Serikali Tanzania kwa kutekeleza kikamilifu miradi inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, na kuongeza kuwa mradi wa ujenzi wa barabara hiyo utaipa fursa za kiuchumi Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi.

Dkt. Mubiru aliongeza kuwa Benki ya Maendeleo ya Afrika itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kutekeleza miradi mbalimbali ya kimaendeleo kwa faida ya benki hiyo na wananchi kwa ujumla.

Mpaka sasa Benki ya Maendeleo ya Afrika- AfDB, imeikopesha Tanzania zaidi ya dola za Marekani bilioniu 1.9, kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara, maji, nishati ya umeme, elimu, na ujenzi wa masoko ya kisasa.

Imetolewa na;

Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha na Mipango